**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KIPINDI CHA JULAI, 2022 HADI JUNI, 2023**

## 1.0. Utangulizi

Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba ipo upande wa Kaskazini Mashariki ya Mkoa wa Kagera. Halmashauri hii ni moja kati ya Halmashauri mbili zilizounda Wilaya ya Bukoba. Halmashauri ya Manispaa ipo katika latitude **1$^{o}$6'** na **1$^{o}$8' 42**" kusini kidogo tu ya mstari wa Ikweta na kati ya longitude **31$^{0}$16' 12**" na **31$^{0}$18' 54**" mashariki ya mstari wa Greenwich ipo mita 1,100 juu ya usawa wa bahari. Hali hii inafanya Halmashauri kuwa na misimu miwili ya mvua yaani vuli ambayo huanza Septemba na kumalizika Desemba na masika ambayo huanza Machi na kumalizika Juni. Kipindi cha Julai hadi mwanzoni mwa Septemba ni kiangazi na kipupwe huanza Januari hadi Februari. Halmashauri ya Manispaa kwa upande wa Mashariki na Ziwa Victoria na pande zingine zote imezungukwa na Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba. Wastani wa mvua kwa mwaka ni milimita 1,200 ambazo hufanya mimea kuwa na kijani kwa mwaka mzima.

### 1.1. Eneo

Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba ina ukubwa wa kilometa za mraba 105 kati ya hizo, kilometa za mraba 22 zimefunikwa na maji ya Ziwa Victoria na eneo lililobaki la kilometa za maraba 83 ni nchi kavu. Kimkoa eneo la Manispaa Bukoba ni sawa na 0.28% ya eneo lote la Mkoa wa Kagera ambalo ni kilometa za mraba 40,838.

### 1.2. Vipaumbele

Halmashauri ilijikita katika kuhakikisha inakabiliana na changamoto zifuatazo:-

1.2.1 Umasikini
1.2.2 Tatizo la ukosefu wa ajira hasa kwa vijana
1.2.3 Rushwa na ubadhirifu wa mali za umma
1.2.4 Uvunjifu wa amani na usalama

Katika kutekeleza shughuli za Serikali, Halmashauri inazingatia pia dhima na malengo yaliyowekwa katika:-

1.2.5 Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020/2025
1.2.6 Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025
1.2.7 MKUKUTA
1.2.8 Malengo ya Millenia
1.2.9 Sera za sekta mbalimbali

### 1.3. Hali ya Ulinzi na Usalama

Kwa kipindi chote cha Julai, 2022 hadi Juni, 2023 hali ya Ulinzi na Usalama kwa Wilaya ya Bukoba iliendelea kuimarishwa. Aidha matukio makubwa na madogo ya uhalifu kwa kipindi hiki yalidhibitiwa vilivyo na vyombo vyetu vya dola kwa kushirikiana na wananchi.

## 2.0. UKUSANYAJI MAPATO

Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba kwa mwaka 2022/2023 iliidhinishiwa kukusanya, kupokea na kutumia jumla ya shilingi **32,083,434,000.00** kutokana na Ruzuku toka Serikali Kuu, Wahisani, Mapato ya ndani na Wananchi kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za kawaida na maendeleo. Hadi tarehe 30 Juni, 2023 Halmashauri ilikuwa imekusanya na kupokea jumla ya shilingi **28,437,569,034.07** sawa na asilimia **89** ya lengo.

Aidha, makusanyo ya mapato ya ndani iliidhinishwa **Tsh.3,520,000,000.00** na zimekusanywa jumla ya **Tsh.3,268,278,182.91** sawa na asilimia **93**. Rejea jedwali hapa chini:-

**Jedwali Na. 1. Mapato na Matumizi halisi hadi tarehe 30 Juni, 2023.**

| Chanzo | Bajeti iliyoidhinishwa | Mapato | % | Matumizi | % |
|---|---|---|---|---|---|
| Vyanzo vya Ndani vya Halmashauri | 2,442,000,000.00 | 2,564,988,121.77 | 105 | 2,446,767,798.99 | 95 |
| Michango mbalimbali Shule za Sekondari | 612,481,038.00 | 272,663,481.33 | 45 | 272,663,481.33 | 100 |
| Ada ya Taka | 200,000,000.00 | 130,553,126.25 | 65 | 130,553,126.25 | 100 |
| Uchangiaji wa huduma ya Afya | 265,518,962.00 | 300,073,453.56 | 113 | 300,073,453.56 | 100 |
| **Jumla ya Mapato ya ndani** | **3,520,000,000.00** | **3,268,278,182.91** | **93** | **3,150,057,860.13** | **96** |
| Ruzuku ya Mishahara | 19,268,632,000.00 | 17,161,185,920.00 | 89 | 17,161,185,920.00 | 100 |
| Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC) | 712,664,000.00 | 801,734,859.00 | 112 | 794,833,859.00 | 99 |
| Ruzuku ya maendeleo na Wahisani | 8,582,138,000.00 | 7,206,370,072.16 | 84 | 7,201,405,067.16 | 99 |
| **Jumla Kuu** | **32,083,434,000.00** | **28,437,569,034.07** | **89** | **28,307,482,706.29** | **99** |

**Jedwali Na.2. Matumizi ya Fedha za Bakaa kwa mwaka 2021/2022.**

| Na | Maelezo | Akaunti | Bakaa | Matumizi | Baki |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Utawala - Ununuzi wa Pikipiki | LGAS – Development | 47,065,416.00 | - | 47,065,416.00 |
| 2 | Afya - Lishe & kulipa deni | LGAS – Development | 5,900,000.00 | 5,900,000.00 | - |
| 3 | Elimu Sekondari - Ujenzi | LGAS - General Fund | 114,683,972.00 | 61,965,416.00 | 52,718,556.00 |
| 4 | Mfuko wa Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu | LGAS – Development | 53,030,283.87 | 53,030,283.87 | - |
| 5 | Elimu Sekondari - Mock | Deposit | 28,029,692.55 | 28,029,692.55 | - |
| 6 | Elimu Msingi - Mock | Deposit | 14,716,489.30 | 14,716,489.30 | - |
| 7 | Elimu Sekondari - UMISETA | Deposit | 4,701,000.00 | 4,701,000.00 | - |
| 8 | Elimu Msingi – UMITASHUMITA | Deposit | 3,144,308.36 | 3,144,308.36 | - |
| 9 | Elimu Sekondari – P4R | Deposit | 2,682,000.00 | 2,682,000.00 | - |
| 10 | Elimu Msingi – P4R | Deposit | 13,310,557.64 | 13,310,557.64 | - |
| 11 | Development Activities ULGSP NCL | Deposit | 390,434,656.45 | 390,434,656.45 | - |
| | **Jumla** | | **677,698,376.17** | **577,914,404.17** | **99,783,972.00** |

**Jedwali Na.3. Matumizi ya fedha za Mapato ya Ndani hadi tarehe 30 Juni, 2023**

| Na. | Shughuli | Makisio | Matumizi halisi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Michango mbalimbali Shule za Sekondari | 612,481,038.00 | 272,663,481.33 | 45 |
| 2 | Ada ya Taka | 200,000,000.00 | 200,000,000.00 | 100 |
| 3 | Uchangiaji Huduma ya Afya | 265,518,962.00 | 300,073,453.56 | 100 |
| 4 | Malipo ya Mishahara | 26,187,000.00 | 25,885,685.22 | 99 |
| 5 | Miradi ya Maendeleo | 732,600,000.00 | 728,818,081.50 | 99 |
| 6 | Mfuko wa Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu | 244,200,000.00 | 244,200,000.00 | 100 |
| 7 | Matumizi Mengineyo | 1,439,013,000.00 | 1,378,417,158.52 | 96 |
| | **Jumla** | **3,520,000,000.00** | **3,150,057,860.13** | **89** |

**Mafanikio**

Halmashauri imefanikiwa kupata **Hati Safi** kwa Hesabu za Fedha za mwaka 2021/2022 zilizokaguliwa na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG).

## 3.0. UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

### 3.1. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III)

Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba kwa mwaka 2022/2023 imepokea na kuwezesha malipo ya **Tsh.657,023,535.00** kwa ajili ya ruzuku kwa kaya maskini **3136** kutoka katika mitaa **65** inayotekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini, fedha hii imewanufaisha walengwa katika Nyanja mbalimbali ikiwemo kukarabati nyumba, ufugaji, kilimo**,** biashara, ufundi na kuanzisha miradi ya kuinua kipato.

Pia mpango wa uundaji wa vikundi vya kijamii kutoka kwa walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini umefanyika katika mitaa 45 ambapo jumla ya vikundi vya kijamii 142 vyenye wanachama 1168 wakike wakiwa 1062 na wakiume 106 vimeundwa na vimeanza mchakato wa kupata usajili ili viweze kunufaika na fursa mbalimbali za mikopo ya Serikali na kutoka katika taasisi za fedha.

Aidha, Mafunzo ya kujengea uwezo yametolewa kwa viongozi 568 wa vikundi vya kijamii 142 ambao wamepatiwa mafunzo ya taratibu za usajili wa vikundi na namna ya kutumia fulsa za kifedha kuimarisha vipato vya wanakikundi hadi sasa vikundi 21 vimesajiliwa katika mfumo wa kielektroniki wa wizara.

### 3.2. Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri imetoa jumla ya **Tshs.244,200,000.00** ambazo ni 10% ya mapato ya ndani kwa ajili ya mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kiasi cha Tshs.150,000,000.00 zilikopeshwa kwa vikundi 15 kama vifuatavyo:-

| Na | Kikundi | Idadi | Kiasi |
|---|---|---|---|
| 1 | Wanawake | 08 | 77,000,000.00 |
| 2 | Vijana | 05 | 63,000,000.00 |
| 3 | Wenye ulemavu | 02 | 10,000,000.00 |
| | **Jumla** | **15** | **150,000,000.00** |

Aidha, itakumbukwa kuwa tarehe 13/4/2023 Waziri Mkuu alitoa agizo kwa nchi nzima kusitisha zoezi la ukopeshaji mikopo ya asilimia 10% mpaka hapo Serikali itakapotoa utaratibu mpya wa ukopeshaji mikopo, hivyo kiasi cha Tshs.94,200,000.00 kipo kwenye akaunti ya mfuko wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

### 3.3. Utekelezaji wa shughuli za Idara ya Maendeleo ya Jamii na Vijana

Kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 Idara imefanya shughuli zifuatazo:-

(i) Kuwezesha usajili wa vikundi vya kijamii na huduma ndogo za kifedha

(ii) Kutembelea na kukagua vikundi vilivyoomba mikopo pamoja na kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vikundi 77 vyenye wanachama 602 (wanawake 504, vijana 84 na watu wenye ulemavu 14).

(iii) Kufuatilia marejesho ya mikopo ya vikundi ambapo jumla ya Tsh.255,984,900 zimerejeshwa

(iv) Kuratibu shughuli za kimtambuka na sherehe za kitaifa ikiwa ni pamoja na;

- Siku ya wanawake Duniani na siku ya mtoto wa Afrika Dunian
- Siku ya familia
- Siku ya wajane pamoja na siku ya UKIMWI Duniani.
- Kutoa Elimu kwa jamii kuhusiana na kushiriki kwenye miradi ya Maendeleo katika maeneo yao wanayoishi hasa mradi wa BOOST
- Kuelimisha jamii umuhimu wa kuchangia lishe kwa watoto walioko shuleni

## 4.0. HUDUMA ZA KIUCHUMI

### 4.1. KILIMO

Upatikanaji wa chakula kwa Mwaka 2022/2023 (Julai 2022 – Juni 2023) ulikuwa mzuri, mahitaji yalikuwa ni tani 53,627 na upatikanaji ni tani 63,150 na ziada ni tani 9,523.

a) Kutoa ushauri kwa wakulima 2,358 kuhusu kuzingatia kanuni bora za kilimo ambapo jumla ya hekta 1,909 zimepandwa na tani 16,511 za mazao ya chakula, biashara, mboga na matunda zimevunwa.

b) Kusajili wakulima 625 kwenye mfumo wa mbolea za ruzuku wa Serikali ambapo wakulima wanatumiwa namba za utambulisho kwa ajili ya kuuziwa mbolea kwa bei ya ruzuku. Hata hivyo kutokana na Manispaa kukosa wakala, wakulima wanaelikezwa kununuwa mbolea kwa mawakala waliopo nje ya Manispaa kama Kemondo na Missenyi.

c) Kufanya maandalizi ya vipando (demo plots) na kushiriki Maonesho ya wakulima (Nanenane) Mwaka 2022 ngazi ya Mkoa katika viwanja vya Maonesho ya Kyakailabwa

d) Kutoa mafunzo ya kanuni bora za kilimo cha mazao ya bustani katika vikundi viwili vya shamba darasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba (green house) Mtaa wa Kyakailabwa

e) Kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa bei za mazao sokoni kila wiki na kutoa taarifa kwa wadau mbalimbali.

f) Kufanya ukaguzi wa maduka ya pembejeo za kilimo 6 yanayouza mbalea kwa kushirikiana na wakaguzi wa mamlaka ya mbolea Tanzania (Tanzania Fertilizer Regulatory Authority (TFRA).

g) Kuhamasisha kilimo cha zao la vanilla kwa wakulima 105 ambapo jumla ya kilo 1,838.59 zenye thamani ya Tsh. 55,157,700.00 zimenunuliwa kwa wakulima 83 na Halmashauri kupata ushuru wa Tsh.1,654,731.

h) Kuhamasisha kilimo cha zao la parachichi aina ya hass kwa wakulima kupitia maonesho ya Nane Nane 2022 na Maafisa Ugani kila Kata. Aidha jumla ya vitalu vya miche ya parachichi vitano (5) vimeanzishwa na wakulima katika Kata za Kitendaguro, Kibeta, Nyanga na Nshambya ambao walipewa mafunzo kupitia taasisi ya usajili wa mbegu Tanzania (TOSCI). Aidha vitalu hivyo vina jumla ya miche ya parachichi aina ya hass takribani 10,000 inayotarajiwa kuuzwa kwa wakulima katika kipindi cha Mwaka 2023/2024.

### 4.2. MIFUGO NA UVUVI

#### 4.2.1. MIFUGO

Halmashauri imeendelea kutekeleza shughuli za mifugo kama ifuatavyo:-

a) Idadi ya mifugo iliyowekewa hereni za kielektroniki ni ng'ombe 190 na mbuzi 73.
b) Utoaji wa chanjo kwa mbwa 402 na paka 24 dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa na paka. Pia mbwa 7 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa DHLP. Aidhat, uthibiti wa magonjwa ya kuku umefanyika kwa kuchanja kuku 34,766 dhidi ya kideri na kuku 7,868 dhidi ya ugonjwa wa ndui na kuku 2,747 dhidi ya gumboro.
c) Kuhamasisha wananchi kujiunga katika vikundi, ambapo jumla ya vikundi vipya 2 vya ufugaji kuku vimebainiwa katika kata ya Kashai. Kutoa elimu ya ufugaji wa ndani hasa katika mitaa ya mjini ili kuepusha migogoro kati ya majirani.
d) Pia Halmashauri ya Manispaa Bukoba inaendelea kusimamia mnyororo wa thamani wa zao la maziwa ambapo kiasi cha wasitani wa lita 4,432 zinazalishwa kwa siku. Bei ya maziwa kwa lita ni wasitani wa Tsh 1,200.
e) Idadi ya ng.ombe 381 wamehimilishwa ili kuboresha kosafu za mifugo kuongeza uzalishaji wa maziwa.

#### 4.2.2. UVUVI

Utekelezaji wa shughuli za Uvuvi ni kama ifuatavyo:-

a) Elimu ya ufugaji wa samaki inaendelea kutolewa ambapo jumla ya wananchi 190 wamehamasishwa juu ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba
b) Mitumbwi 167 imesajiliwa na kulipia leseni za uvuvi
c) Elimu kuhusu athari za uvuvi haramu imetolewa kwa jamii ya wavuvi na inaendelea kutolewa ambapo jumla ya doria 18 zimefanyika na kukamata zana haramu ambazo ni kokoro 2 za sangara, nyavu za timba 80, samaki wachanga kilo 680 pamoja na watuhumiwa 4
d) Kikundi kimoja (01) cha uvuvi cha Rise and Community Service kimefanikiwa kupewa mkopo wa Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya ufugaji wa samaki kwa njia ya Vizimba.

## 5.0. MALIASILI NA MAZINGIRA

### 5.1. Mazingira

a) Jumla ya miti **33,845** imepandwa katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba.
b) Kuhamasisha wananchi kupanda miti ya matunda, mapambo na maua kwa ajili ya upendezeshaji mji (Town beautification) ambapo *Palm trees* imepandwa kandokando ya barabara za mjini kati
c) Kutoa elimu juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji na kubainisha vyanzo 113 kwa kushirikiana na wananchi waliokaribu na vyanzo husika.

### 5.2. Ufugaji Nyuki

a) Kutoa elimu ya uvunaji na uchakataji wa asali na nta katika vikundi 3 vya ufugaji nyuki vilivyopo Manispaa ya Bukoba (UKU- Ntungamo Buhembe, Tweyambe Ijuganyondo A na Tweyememu Bugambakamoi)
b) Kutembelea na kutoa elimu kwa wafugaji nyuki binafsi 5 (Ijuganyondo 2, Buhembe 1 na Kitendaguro2)
c) Kuwezesha utoaji wa nyuki katika jengo la zahanati ya Buhembe.
d) Kufanya makabidhiano ya mashine ya kuchakata asali
e) Kufanya usimamizi wa shughuli za Ufugaji nyuki

### 5.3. Usimamiziwa wa Taka na Usafi wa Mazingira

Hali ya Usafi na Mazingira mji wa Bukoba ni ya kuridhisha. Halmashauri ina magari mawili ya kusafirisha taka ngumu aina ya Tipper za tani 8 kila moja na mtambo wa kuzolea taka (backhole wheelloader).

a) Jumla ya tani 9,200 za taka ngumu zilizolewa katika vizimba vyote 25 na zimetupwa katika dampo kuu la Nyanga.
b) Jumla ya marehemu 62 wasiojulikana na wasio na Ndugu au jamaa walizikwa
c) Kumefanyika uondoaji mchanga na tope katika barabara zote za katikati na pembezoni mwa Mji
d) Wananchi wamekuwa wakishiriki usafi wa mazingira kila Alhamisi na Jumamosi ya kila wiki kwa kata 14 na mitaa 66 ya Manispaa ya Bukoba.
e) Ukaguzi wa mazingira umefanywa kwenye maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Bukoba na jumla ya ilani 624 zimetolewa kwa majengo ya makazi/biashara/taasisisi zilizohitajika marekebisho.
f) Ufyekaji wa nyasi umefanyika kwenye maeneo ya wazi kama vile roundabout ya Stand kuu, Uwanja wa Mayunga, ELCT-Tea room, Udhibiti Ubora wa Elimu – BMC, Mahakama Kuu/Mkoani – Kasarani

## 6.0. ARDHI NA MIPANGO MIJI

Shughuli zilizotekelezwa kwa mwaka fedha 2022/2023 ni kama ifuatavyo:-

i) Hatimiliki zilizoandaliwa ni 1406. Pia maombi ya kumilikishwa ardhi 1246 yamepokelewa.
ii) Jumla ya migogoro 23 ya ardhi imetatuliwa
iii) Makusanyo ya kodi ni Tshs.560,963,587.98
iv) Viwanja vilivyopimwa ni 88 vya watu binafsi na 3 vya Taasisi. Pia jumla ya viwanja vya urasimishaji 25,508 vimepimwa. Aidha jumla ya viwanja 282 vimeoneshwa mipaka.
v) Vibali vya ujenzi 218 vimetolewa. Pia jumla ya ‘deedplans’ 663 zimechorwa.

## 7.0. HUDUMA ZA JAMII

### 7.1. MFUKO WA JIMBO

Halmashauri ya Manispaa ilipokea jumla ya fedha **Tshs.58,926,000.00** za Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya kuchochea miradi ya maendeleo katika Jimbo la Bukoba Mjini. Kiasi cha Tshs.40,000,000.00 kiliielekezwa kufanya shughuli ya ufunguzi wa barabara katika kata ya Kibeta, Bakoba, Nyanga, Kahororo na Nshambya ambapo kazi imekamilika na kiasi cha Tshs.8,926,000.00 kimetumika kutengeneza boti katika kata ya Miembeni. Aidha, Tshs.10,000,000.00 ipo kwenye akaunti ya kata Miembeni na itatumika itakapopangiwa shughuli ya kufanya na kamati ya mfuko wa Jimbo.

### 7.2. ELIMU YA AWALI NA MSINGI

a) Kuratibu na kusimamia mitihani ya kumaliza Elimu ya msingi 2022 kwa wanafunzi **3,686** kwa shule 42 ambapo wasichana walikuwa **1,807** na wavulana **1,879.**
b) Kuratibu na kusimamia upimaji wa Kitaifa darasa la Nne 2022 kwa wanafunzi **3,903** kwa shule 45 ambapo wasichana walikuwa **1,979** na wavulana **1924.**
c) Kufanya uchunguzi kwa wanafunzi wenye matatizo ya uoni katika shule za msingi za serikali.
d. Kuratibu zoezi la upokeaji na uandikishaji wa wanafunzi **2,860** (wavulana **1,452** wasichana 1,466) wa awali na wanafunzi **3,530** (wavulana **1,784** wasichana **1,746**) wa darasa la kwanza
e. Kusimamia matumizi sahihi ya fedha za Elimu bila malipo**Tsh.415,052,292** zilizopokelewa kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023.
f. Kuratibu shughuli za usajili wa madarasa ya mitihani darasa la saba na darasa la nne ambapo darasa la saba wamesajiliwa jumla ya wanafunzi 4,167(wavulana 2,078,wasichana 2,089) na darasa la nne

wanafunzi 3,839 (wavulana 1900, wasichana 1939) wamesajiliwa na wanategemewa kufanya mtihani mwaka huu 2023.

g. Kusimamia utoaji wa chakula na lishe kwa shule zote 25 za Serikali na shule 23 za Binafsi. Hata hivyo idadi ya wanafunzi wanaopata chakula ni ni asilimia 43 kwenye shule za Serikali na asilimia 100 kwa shule za Binafsi. (Rejea Kiambatisho)

h. Kuimarisha club za afya na Lishe kwa shule zote 48 za msingi Serikali na Binafsi kwa kuzitembelea na kutoa mwongozo kwa walimu wa afya.

i. Kusimamia ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi 6 kupitia mradi wa BOOST kwa Tsh.1,059,600,000.00 katika shule za msingi Ihungo, Kiteyagwa, Rwemishasha, Rwemishasha B, Rumuli na shule mpya ya Mafumbu B, pamoja na ukarabati wa miundombinu ya shule ya msingi Bunena kwa Tsh.100,000,000.00 za mradi wa EP4R.

j. Uelimishaji na uhamasishaji wa kujikinga na ugonjwa wa Marbug katika shule zote za serikali na binafsi kwa asilimia 100.

k. Uhamasishaji wa watoto wenye ulemavu katika kata 14 kuandikishwa shule.Jumla ya watoto 33 wavulana 12 na wasichana 11 wenye umri wa kuanza shule waliandikishwa katika shule maalumu, vitengo na shule jumuishi.

l. Kuratibu na kusimamia malipo ya nauli kwa walimu 104 ambapo kiasi cha Tsh. 21,755,200.00 na Fedha za matibabu kwa walimu 32 Tsh. 38,861,990.00 zililipwa.

m. Kuratibu zoezi la ufanyikaji wa mitihani ya mock mkoa darasa la saba 2023 ambapo jumla ya wanafunzi 4051 (wavulana 2,002 na wasichana 2,049) walifanya mtihani huo. Usahihishaji ulifanyika katika Chuo cha Ualimu Katoke na ufaulu ulikuwa asilimia 97.2

n. Kuratibu uanzishwaji wa mchepuo wa kiingereza katika shule ya msingi Rumuli iliyoanza Januari 2023 ambapo jumla yawanafunzi 288 (wavulana 139,wasichana 149) wamesajiliwa kuanza masomo kwa mchepuo wa kiingereza. Shule itaendelea kusajili wanafunzi wa elimu ya awali na darasa la kwanza kwa mfumo wa kiingereza kila mwaka na wanafunzi wa mfumo wa Kiswahili waliopo wataendelea na masomo hadi watakapohitimu wote na kubaki na mfumo wa kiingereza pekee.

### 7.3. ELIMU YA SEKONDARI

a) Kuratibu mapokezi na kuwasajiri wanafunzi wa kidato cha **kwanza, 2023** Walichanguliwa kujiunga na kidato cha kwanza ni wanafunzi **3421**

b) Kuratibu na kusimamia mitihani ya utimilifu Mkoa (MOCK) kwa kidato cha Pili, Nne na kidato cha Sita 2023.

c) Kuratibu na kusimamia mtihani wa Taifa kidato pili na cha Nne (CSEE) Novemba 2022 na kidato cha Sita (ACSEE) Mei, 2023.

d) Kuratibu fedha za Elimu bila malipo jumla ya **Tsh.2,419,226,803.66.**

e) Kusimamia ujenzi wa vyumba 49 vya madarasa ya kidato cha kwanza 2023 katika Shule za Sekondari; Bakoba (6), Bilele (5), Buhembe (3), Bukoba (2), Hamugembe (2), Ijuganyondo (2), Kashai (12), Kibeta (1), Nshambya (4), Nyanga (2), Rugambwa (1), Rumuli (1), Rwamishenye (6) na Rwazi (2) kwa Tshs.980,000,000.00 toka Serikali Kuu. Ujenzi umekamilika.

f) Kusimamia ujenzi wa Bweni katika Shule ya Sekondari Kagemu kwa kiasi cha Tshs.100,000,000.00 kwa fedha za SEQUIP, Jengo lipo hatua ya ukamilishaji. Aidha, fedha iliyoletwa haikutosha, hivyo Halmashauri imefanya tathimini ya Tsh.49,318,390.00 ambayo itatolewa kutoka mapato ya ndani ili kukamilisha mradi.

g) Kusimamia ujenzi wa Bweni, madarasa 4 na vyoo matundu 7 katika Shule ya Sekondari Kahororo kwa ufadhili wa *Barick Gold Mining* kwa kiasi cha Tshs.244,700,000.00 ambayo inatosha kukamilisha mradi. Bweni lipo katika hatua ya renta, vyoo na madarasa vipo katika hatua ya umaliziaji.

h) Kusimamia ujenzi wa Mabweni 4, madarasa 7 na vyoo matundu 10 katika shule ya sekondari Omumwani kwa **Tshs.716,000,000.00** toka Serikali Kuu. Madarasa ya yamekamilika na yanatumika, Mabweni na vyoo vipo hatu ya ukamilishaji. Aidha, fedha iliyopo haitoshi hivyo tathimini inaendelea kufanyika ya gharama zitakozohitajika kukamilisha mradi.
i) Mapokezi ya fedha kiasi cha **Tshs.584,280,028.00** kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya Kata ya Kagondo. Maandalizi ya hatua za awali, kuunda kamati za kusimamia ujenzi pamoja na taratibu za manunuzi zinaendelea.
j) Mapokezi ya fedha kiasi cha **Tshs.100,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mwalimu katika shule ya Sekondari Samia Suluhu. Shule hii ilifungulia Januari, 2023 hivyo ina upungufu wa miundombinu. Aidha, maandalizi ya hatua za awali, kuunda kamati za kusimamia ujenzi pamoja na taratibu za manunuzi zinaendelea.
k) Kusimamia ujenzi wa matundu 24 ya vyoo katika Shule ya Sekondari Kashai kwa kiasi cha Tshs.14,700,000.00 kwa fedha za TEA. Shule hii ilikuwa na upungufu mkubwa wa matundu ya vyoo

**Mafanikio**

- Manispaa ya Bukoba ilishika nafasi ya 1 kimkoa kwa ufaulu wa asilimia 92.8 katika mtihani wa kidato cha IV 2022.
- Pia katika mtihani wa kidato cha sita 2023 Manispaa ya Bukoba ilishika nafasi ya 1 Kimkoa kwa ufaulu wa asilimia 98.

### 7.4. AFYA

Kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 Idara imefanya shughuli zifuatazo:-

a) Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Nshambya unaendelea kufanyika ambapo jengo la Wagonjwa wa nje (OPD), maabara na jengo la kufulia yamekamilika. Jengo la wodi ya mama na mtoto pamoja na wodi ya Wanaume na Wanawake yapo hatua ya ukamilishaji. Hata hivyo jengo la wagonjwa wa nje limeanza kutoa huduma tangu mwezi Machi 2023. Aidha kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kituo kimetengewa bajeti ya Tsh.800,000,000.00 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kuendeleza ujenzi.

b) Kununua dawa, vitendanishi na vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya kutoa huduma za afya.

c) Kufanya usimamizi shirikishi kwenye vituo vyote vya kutolea huduma

d) Kufanya utekelezaji wa Kampeini endelevu ya utoaji wa chanjo za UVIKO-19 katika vituo vyote 11

e) Kufanya kliniki za huduma za mkoba na huduma tembezi vituoni.

f) Kusambaza chanjo katika vituo vyote 11 vinavyotoa huduma ya chanjo ndani ya Wilaya

g) Utekelezaji wa kampeini ya kutokomeza POLIO mbapo katika round ya pili jumla ya waliochanjwa ni 35,726 ambayo ni asilimia 132.5%, katika round ya tatu jumla ya waliochanjwa ni 38,155 sawa na asilimia 106.8% na round ya nne jumla ya waliochanjwa ni 149,900 sawa na asilimia 107.2%

h) Kufanya ukaguzi wa matumizi ya dawa vituoni

i) Uhamasishaji wa uchangiaji wa damu salama ambapo jumla ya chupa 681 zimepatikana na mahitaji kwa mwaka ni chupa 600 hivyo kuvuka lengo.

j) Kufanya usimamizi shirikishi vituoni kufuatilia matumizi sahihi ya kipimo cha Maralia (MRDT) na kwa mwaka 2022/2023 kiwango cha maralia ni 5.1%

## 8.0. MASUALA MTAMBUKA

### 8.1. MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI

a) Uhamasishaji na kutoa huduma ya tohara kwa wanaume 1500

b) Kutoa mafunzo kwa watumishi 75 kutoka vituo 12 vya kutolea huduma za Tiba na Matunzo (CTC) na vituo 4 vya huduma ya uzuiaji wa maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT) juu ya matibabu sahihi ya watoto wanaoishi na VVU.

c) Kutoa huduma ya Jipime ambapo wateja 7,901 wamepewa vitepe vya jipime na kati yao wateja 7,896 sawa na 99% wamerudisha majibu. Aidha kati yao wateja 174 sawa 2% walikuwa na viashiria vya maambukizi ya VVU.

d) Kufanya upimaji wa VVU katika vituo 17 vya kutolea huduma za Afya. Jumla ya wateja 36,691 (Me 10,903 na Ke 25,788) wamepimwa VVU. Kati yao wateja 1,032 (Me 346 na Ke 686) sawa na 2.8% walipatikana na maambukizi ya VVU na kuunganishwa kwenye kliniki ya Tiba na matunzo.

### 8.2. VITA DHIDI YA MALARIA NA KIFUA KIKUU

a) Elimu ya kujikinga na maambukizi ya malaria imetolewa kwa jamii katika mitaa yote 66

b) Vyandarua **29,498** zimegawiwa kwa mama wajawazito , watoto chini ya umri wa miaka mitano wanaopata chanjo ya kwanza ya surua (miezi tisa) na wanafunzi wa shule za msingi 45

c) Upimaji wa vimelea vya malaria umefanyika kwa watu 93,251 (Me 37,672 na Ke 55,579) na watu 4795 wamekutwa na vimelea vya malaria sawa na 5.1.% na wakaanzishiwa matibabu bure

d) Uchunguzi wa Kifua Kikuu katika Magereza ya Bukoba umefanyika mara 3 ambapo jumla ya sampuli 64 zilikusanywa na kupimwa na wagonjwa 3waliibuliwa, Aidha uchunguzi wa Kifua kikuu katika maeneo hatarishi hasa maeneo ya makazi ya wavuvi umefanyika mara mbili. Pia uchunguzi ulifanyika katika maeneo ya masoko ambapo jumla ya wagonjwa 472 waliibuliwa na kuanzishiwa matibabu bila malipo.

### 8.3. WAZEE

Jumla ya wazee **2682** ambapo Ke ni 1,673 na Me ni 1,009 walio na umri kuanzia miaka 60 na kuendelea wametambuliwa katika mitaa yote 66, na wazee **2594** wamepatiwa vitambulisho vya kupata matibabu bila malipo.

Vituo na zahanati vimeendelea kutoa huduma za Afya bure kwa wazee kama sera ya Afya inavyoelekeza. Aidha, watumishi wa sekta ya Afya wametakiwa kuhakikisha wanatoa kipaumbele kwa wazee.

### 8.4. UTAWALA BORA

a) Kuratibu vikao vya Kisheria vya CMT, Kata, Mitaa na Baraza la Madiwani

b) Kusimamia ulipaji wa posho kwa Wenyeviti wa Mitaa kwa kila mwezi

c) Kuajiri watumishi 22 na kubadilisha / kupandisha kada/ madaraja watumishi 194

d) Kusimamia ulipaji wa mishahara pamoja na posho za wahen.Madiwani kila mwezi

e) Kusimamia ulipaji wa posho za Madaraka kwa Watendaji wa Kata 14 kila mwezi

f) Jumla ya watumishi 194 waliostahili kupandishwa vyeo wamepandishwa vyeo na kupewa barua zao za kupandishwa vyeo.

g) Kuratibu watumishi wanaohama na kuhamia Halmashauri ya Manispaa Bukoba, ambapo watumishi 26 wamehamia na 23wamehama

h) Mashauri ya kinidhamu kwa watumishi saba (7) yametolewa na yanaendelea katika hatua za maamuzi kwa mujibu wa sheria na kanuni za utumishi wa Umma.

i) Kero 30 za wananchi zimepatiwa ufumbuzi.

j) Halmashauri ilipata misiba mitatu (3) ya watumishi ambapo mmoja ni Idara ya Elimu, mmoja ni idara ya Utawala na mmoja Idara ya Afya.

### 8.5. MAENDELEO YA MICHEZO NA UTAMADUNI

Shughuli zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni kama ifuatavyo:-

a) Utoaji wa vibali vya burudani pamoja na Uwanja wa Kaitaba ambapo jumla ya **Tsh.10,402,808.96** zimekusanywa sawa na **103%** za makusanyo.

b) Kuandaa mashindano ya UMISSETA na UMITASHUMTA kuanzia ngazi ya shule hadi Kitaifa Mkoani Tabora.

c) Kitengo kimeandaa na kuratibu mapokezi ya Mwenge wa Uhuru mwaka 2023.

d) Kuandaa na kuratibu sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

e) Kuratibu na kusimamia matamasha mbalimbali ya michezo na Utamaduni kama vile Kasibate festival, Kagera festival, Kagera awards, Senene festival, Zagwa boxing day (Bonanza la ngumi) TAKUKURU rafiki, Elimu ya Mlipa kodi na mabonanza mengine ya taasisi mbalimbali.

f) Kuratibu program za maendeleo ya michezo kwa vijana katika Uwanja wa Kaitaba.

### 8.6. VITA DHIDI YA RUSHWA

Mapambano dhidi ya RUSHWA yanaendelea, watumishi na wananchi wameelimishwa madhara ya rushwa na wametakiwa wasiombe, kutoa wala kupokea rushwa na yeyote atakayedhibitika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.  Ili suala hili kuwa endelevu elimu imefikishwa mpaka kwenye shule za msingi na sekondari.

## 9.0. MIRADI YA UWEKEZAJI NA MIRADI YA KIMKAKATI YA KUONGEZA WIGO WA MAKUSANYO YA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI

1. **Mradi wa Upendezeshaji Miji - TACTIC**

Manispaa ya Bukoba ipo katika awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi wa TACTIC ambapo miradi iliyopendekezwa na kupitishwa kwa ajili ya kutekelezwa ni pamoja na ifuatayo:-

- i) Ujenzi wa stendi mpya ya mabasi – Kyakailabwa
- ii) Ujenzi wa soko Kuu jipya la Bukoba mjini
- iii) Ujenzi wa kingo za mto Kanoni ndani ya mji wa Bukoba
- iv) Uwekaji taa za barabarani kwenye barabara za Bukoba mjini
- v) Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami Bukoba mjini

**Hatua iliyofikiwa kwa Sasa**

- Timu ya Wataalam kutoka TAMISEMI ilikuja tarehe 26/6/2023 kwa ajili kutoa maelekezo ya uandaaji wa taarifa za awali za miradi itakayotekelezwa.
- Uundaji wa timu ya Manispaa itakayoshiriki katika kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi.
- Maandalizi ya taarifa za awali za miradi itakayotekelezwa. Aidha inategemewa kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/24 kazi ya usanifu wa miradi itaanza kufanyika.

2. **Mradi wa Maegesho ya Magari Makubwa.**

Mradi wa maegesho ya malori uliwekwa jiwe la msingi na Mkuu wa Mkoa Kagera, Mhe. Albert Chalamila tarehe 13/3/2023 baada ya kukamilika kwa ujenzi awamu ya kwanza. Aidha mradi utaanza kutumika baada ya kutekeleza maagizo ya Mkuu wa Mkoa.

3. **Ujenzi wa Soko la Ndizi Kagondo**

Eneo la ujenzi wa soko limeshazawazishwa na kuwekewa moramu pamoja na ujenzi wa mitaro. Pia ujenzi wa choo umekamilika. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 zimetengwa jumla Tsh. 10,000,000.00 kwa ajili ya kujenga mabanda.

4. **Ujenzi wa Ofisi wa Wamachinga ya Mkoa**

Ofisi ya Wamachinga ya Mkoa inajengwa Kata ya Kashai na jengo liko hatua ya usawa wa lenta. Jumla ya Tsh.13,500,000.00 zinatumika, ambapo Tsh.10,000,000.00 kutoka Serikali Kuu na Tsh.3,500,000.00 ni mchango wa Manispaa ya Bukoba. Aidha Halmashauri zote za Mkoa Kagera zinapaswa kuchangia.

5. **Miradi mingine ya uwekezaji** ambayo iko kwenye mpango wa Halamashauri wa kuitekeleza ambapo taratibu za kuwapata wataalam wa kufanya usanifu pamoja na kuombea fedha katika taasisi za kifedha zinaendelea:-
   - i) Ujenzi wa Shule Mpya ya Mchepuo wa Kiingereza
   - ii) Ujenzi wa Soko la Dagaa
   - iii) Ujenzi wa Ukumbi wa Kisasa

## 10.0. HITIMISHO

Kwa niaba ya wananchi wa Manispaa ya Bukoba tunamshukuru Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha nyingi za maendeleo kwa Manispaa ya Bukoba, Mwenyezi Mungu azidi kumlinda na kumpa maisha marefu aendelee kuwatumikia wananchi, kupitia falsafa ya "***KAZI IENDELEE"***.